UCHUNGUZI LINGANISHI WA MVUTANO KATI YA UKALE NA USASA WA KITAMADUNI ULIOPO KATIKA TAMTHILIA YA KWENYE UKINGO WA THIM NA ULE WA JAMII YA WACHAGA MKOANI MOSHI

NA

NANNONO PAULINE

BAE/43977/143/DU

TASNIFU YA UTAFITI ILIYOWASILISHWA KWENYE IDARA YA LUGHA NA MAWASILIANO KATIKA KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ILI KUKIDHI BAATHI YA MAITAJI YA KUHITIMU SHAHADA YA SANAA NA ELIMU YA CHUO KIKUU CHA KAMPALA INTERNATIONAL UNIVERSITY

AUGUST, 2017

UNGAMO

Mimi Nannono Pauline naungama ya kwamba kazi hii ni yangu mwenyewe na haijashughulikiwa na kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote Sahihi..……

Mtahiniwa; **NANNONO PAULINE**

Tarehe..12/8/2017……

IDHINI

Tasnifu hii ambayo imefanywa na Nannono Pauline imewasilishwa kwa idara ya lugha na sanaa kwa ajili ya kutimiza baadhi ya maitaji ya shahada ya sanaa na elimu na imekubaliwa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na chuo kikuu cha Kampala International University

Sahihi; .....

Bibi Mutenyo Aidah

Tarehe; 30/08/2017

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia shangazi yangu Bi Matilda john, wazazi wangu Bwana Marko John na mama yangu Bi Jackline Marko, rafiki yangu wakaribu Bwana Antony Kawea, mwalimu wangu Bi Mutenyo Aidah kwa usimamizi wake na muongozo wake kwangu

SHUKRANI

Namshukuru Mungu muumba wangu kwa maisha niliyonayo pamoja na afya njema aliyonipa katika kipindi nilichokuwa nafanya utafiti wangu na shughuli zote za kukamilisha utafiti huu.

Pia namshukuru Bi Mutenyo Aidah, mhadhiri katika idara ya lugha kwa kujitolea mhanga kunisimamia na kunisaidia vilevile. Umekuwa mzazi kwangu Mungu akubariki sana.

Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wengine katika idara ya lugha wakiwemo; Bwana Wilson Onyeit, Bi Azabo na Bwana Atukunda Edwin.

Siwezi kutowashukuru wazazi wangu Bwana Marko john na Bi Jackline Marko kwa kunizaa na kunilea, shangazi yangu Bi Matilda john kwa kunikuza, kunitunza, kunilipia karo kuanzia masomo yangu ya sekondari paka hapa nilipo.umekuwa msaada mkubwa kwangu kwani umenilea nakunipenda kama mwanao kuanzia utotoni mwangu paka katika ukubwa wangu, umekuwa rafiki mkubwa kwangu nazaidi ya shangazi sina budi kukuita mama kwani matendo yako nakujitoa kwako kumedhihirisha mengi kwangu, pesa ulizonipatia pamoja na msaada wakati nilipokuwa nafanya utafiti huu nashukuru.

Pia nawashukuru rafiki zangu kama Upendo William. Bwema Kenneth, Ojambo Justine na lukeeyo David.

FAHARASA

UNGAMO i
IDHINI ii
TABARUKU iii
SHUKRANI iv
FAHARASA v
YALIYOMO vii
IKSIRI viii

SURA YA KWANZA 1
1.1 Usuli wa mada 2
1.2 Swala la utafiti 4
1.3 Madhumuni ya utafiti 4
1.4 Malengo mahususi ni; 4
1.5 Umuhimu wa utafiti 5
1.6 upeo wa utafiti 5
1.6.1 Upeo wa kiufundi 5
1.6.2 Upeo wa kijografia 5
1.6.3 Upeo wa kiwakati 5
1.7 Shida zilizomkumba mtafiti 5

SURA YA PILI 7
MAPITIO YA MAANDISHI 7
2.0 Utangulizi 7
2.1 Maandishi kuhusu mila na usasa 7
2.2.1 Maandishi kuhusu jamii ya Wachaga 8
2.4 Maandishi kuhusu mada 10
2.5 Hitimisho 13

SURA YA TATU 14
MBINU ZA UTAFITI 14
3.0 Utangulizi 14
3.1 Utaratibu wa utafiti 14
3.2 Uteuzi wa sampuli 14

3.3 Mbinu za kukusanya data 14
3.4 Hojaji 14
3.5 Mahojiano 15
3.6 Uchunguzi shirikishi 15
3.7 Uteuzi wa vifaa 15
3.8 Uchanganuzi wa data 15

SURA YA NNE 16
UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA 16
4.0 Utangulizi 16
4.1 Uwasilishaji na uchanganuzi wa data 16
4.2 Tathmini ya hojaji na mahojiano 16
4:6 Je majina na methali za kichaga husawili hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa? 20
4.3 Majadiliano ya matokeo 20
4.3.1 Lengo la kwanza 20
4.3.2 Lengo la pili 22
4.3.3 Lengo la tatu 23

SURA YA TANO 26
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 26
5.0 Utangulizi 26
5.1 Muhtasari 26
5.2 Hitimisho 27
5.3 Mapendekezo 28
MAREJELEO 30
VIAMBATANISHO 32

YALIYOMO

Jedwali 4:1 jinsia ya wahojiwa 17
Jedwali 4:2 umri wa wahojiwa 17
Jedwali 4:4 aina za mvutano baina ya mila za zamani na usasa mkoani Moshi; 18
Jedwali 4:5 mvutano wa mila na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim 19
Jedwali 4:3 je unaujuzi na tajriba ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa mkoani humu Moshi? 18

IKSIRI

Utafiti huu umekusudia kuchunguza ulinganishaji wa mvutano kati ya ukale na usasa wa kitamaduni uliopo katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ule wa jamii ya wachaga mkoani moshi.

Malengo ya utafiti huu yalikuwa; kubainisha hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na mvutano wa mila za zamani na usasa ule unaojitokeza katika jamii ya wachaga,kueleza vyanzo vya mvutano wa mila za zamani na usasa kama unavyojitokeza katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na mvutano wa mila za zamani na usasa katika jamii ya wachaga, kubainisha uhusiano kati ya hali hizi mbili yaani mvutano baina ya mila za zamani na usasa, kupendekeza mbinu zakukomesha hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa. Malengo haya yalitimilika kwa kutumia mahojiano, hojaji walizopewa wakazi wa moshi, uteuzi wa sampuli, uchunguzi shirikishi pia vitumiwa katika ukusanyaji wa data. Wahojiwa 40 ndio waliotumiwa kukusanya data hii.

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

Moshi ni mkoa uliopo mashariki mwa Tanzania. Wengi wa wakazi wa jamii hii ni wachaga wakichanganyikana na wapare ambao kabila la wapera wengi wao hukaa kwenye vimilima vya moshi, lakini idadi yao ikiwa ndogo kabisa kulinganisha na wachaga waishio Moshi. Kabila kubwa na lawatu wengi waishio Moshi huitwa chagga au wachaga, ingawa wachaga hawa wamegawanyika katika makundi mbalimbali kama ;Wamachame, Wakibosho, Wakishimundu, Wamarangu, Warombo, Wasiha na Wahuru. Mkoa huu unawakazi wengi zaidi ya watu (185,000) kulingana na sensa ya mwaka (2012).

Mkoa huu umekuwa ni mkoa unaoongoza Tanzania nzima kwa usafi na pia unasifika sana kutokana na kuwepo kwake kwa kivutio cha utalii yaani Mlima Kilimanjaro unaosifika kuwa miongoni mwa milima mirefu Afrika. Hivyobasi kutokana na kuwepo na jamii mbalimbali mkoani Moshi kumekuwa na lugha mbalimbali zinazoongelewa ingawa utamaduni wao umekuwa mmoja yaani "utamaduni wa kichaga" ambao ni mila, desturi, misemo, nyimbo, vitendawili, ngano na vipengele vyote vya utamaduni mahususi.

Vijiji mahususi vya utafiti yaani; Kibororoni, Mwika, Kibosho, na Sambarai ambavyo vinapatikana katika mkoa wa Moshi. Vijiji hivi vina idadi ya watu (4278) na hawa ni pamoja na wanawake, wanaume na watoto. Maisha ya vijiji hivyo niyakawaida yaani familia,ufanyaji wa kazi mbalimbali haswa biashara.

Kwenye "ukingo wa thim"ni tamthilia iliyoandikwa na Ebrahim Hussen (1988). Jina la kitabu "kwenye ukingo wa thim" haswa neno "thim"kwa kijaluo ni "mwitu" lakini kwenye taswira zetu "kwenye ukingo wa thim" linaashiria kua baadhi ya mila za zamani na zinazoabudiwa na jamii zinakaribia kwisha. Tamthilia hii inaonyesha mvutano uliyopo baina ya maitaji ya mila na maitaji ya maisha ya kisasa, hivyo basi tamthilia hii imeonyesha zaidi mvutano huo unavyoweza kutokea na athari zake kwa wanaohusika. Kwa hivyo mtafiti alilinganisha jamii ya watu kwenye tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ile ya Wachaga mkoani Moshi.

1.1 Usuli wa mada

Mtafiti alichunguza mvutano baina ya mila za kale na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ule katika jamii ya Wachaga mkoani Moshi. Mtafiti alipokuwa akisoma tamthilia ya kwenye ukingo wa thim aligundua jamii hiyo imetawaliwa na mvutano baina ya mila za kale na usasa kama vile; ndoa ya Herbart na Martha ambao wanatoka makabila tofauti inavuruga utamaduni kwani mila na desturi za Kiafrikahazimruhusu mtu kuoa nje ya kabila lake. Lakini tumeshuhudia mara nyingi vijana wanapenda kuoa nje ya makabila yao hata kama ndoa hizo huwa zinazuiliwa. Sababu hii inampasa Lydia ukurasa wa 9 kusema " ndio kweli wenyewe siku hizi mambo ya kisasa, kila kitu cha kisasa. Mtazame Herbart na Martha, habari hii yakuoa kabila moja imekwisha kwani kila unayemwona hivyohivyo na hata Chris". Mtafiti alipogundua mvutano huo alilinganisha kazi ya kisanii na hali halisi kwa sababu fasihi haijengeki katika ombwe. Fasihi inatokana na tajriba halisi za binadamu huenda yanayotendeka katika tamthilia hii yanamulika yale yanayotendeka katika jamii halisi ya Wachaga mkoani Moshi. Ili mtafiti aweze kutimiza utafiti wake ilimbidi basi mtafiti achunguze kwa undani ikiwa basi kuna uhusiano wowote kati ya jamii ya Wachaga na ile ya riwayani. Mbali na mvutano wa mila za zamani na usasa kiujumla mtafiti aliposoma kazi kadhaa za wataalam aligundua kwamba kuna swala nyeti la mvutano wa umila na usasa ambalo bado halijachunguzwa vilivyo. Mvutano huu umeenea sana baina ya wapendanao wenye mila tofauti na bila kuzingatiwa vyanzo vyake pamoja na suluhisho maalum, kwa mujibu wa mtafiti hali hii isipochunguzwa kwa umakini huenda matokeo hayatakuwa mazuri kamwe. Mvutano wa aina hii ulijitokeza katika wilaya Nyeza kijiji cha Mweka pale bibi mmoja alipotaka kuolewa na kijana mmoja atokae katika kabila la wapare lakini ndoa yao iliweza kukatawaliwa na wazazi wa binti huyo kwani walidai makabila hayo mawili hayawezi kuoana kwasababu wapare wanasifa ya ufupi hivyo kuna kazi ambazo hawawezi kuzifanya na hata hivyo wapate mara nyingi huwa na sifa ya uvivu na wengi wao huwa maskini kitu ambacho hakikubaliwi na wachaga wengi maana hao huamini katika uchapa kazi na utajiri. Hata hivyo wapenzi hawa wawili waliweza kuoana bila idhini ya wazazi wao na hivyo msichana aliishia kutengwa na jamii yake. Mtafiti aliichukua hali hiyo na kuilinganisha na ndoa ya Herbart na Martha ambayo ilikuwa haikubaliwi kisa ni makabila tofauti.

Herbart anamuoa Martha ambaye wanatoka makabila tofauti na nikitendo ambacho hakiruhusiwi katika mila na desturi yao, hakuishia tu hapo Martha anaolewa akiwa tayari na mtoto amwitae Chris ambaye sio mtoto wa Herbart. Jambo hili linawaudhi sana wanafamilia

wa Herbat kwani nikitendo ambacho hakikubaliki katika jamii yao na mila yao inadhihirisha kitendo hicho kama "haramu" hivyo Chris ambaye ni mtoto wa Martha anaonekana kutengwa nakutopokelewa katika jamii ya wakina Herbat lakini Herbart anamkubali nakumpenda Chris kama mwanae wakumzaa.

Ben kwa upande mwingine ni mtamaduni zaidi na anamchukia dada yake Martha kisa ameolewa na kabila ambalo sio lake na alionekana akiongea maneno yafuatayo " toka uko huyo mke ameolewa na wewe mimi simjui kama dada yangu labda ni bibi yako tu" maneno hayo alisema Ben kwa Herbart ambaye ni shemeji yake. Hivyo basi tunaona ni jinsi ngani mila za zamani na usasa unamvutano mkubwa.

Katika mila na desturi za Kiafrika kuna miiko ambayo huwekwa kwa mtoto wakiume ambaye anataka kuoa na mwenye mafanikio kuwa nilazima ajenge nyumba kijijini kwao ili atakapokufa wapate mahali pa kumzika lakini tunamwona Herbart akipinga jambo hili nakukataa kujenga kijijini nakujenga tu mjini nyumba ya kifahari nayakisasa nahakuishia tu hapo alitaka kwenda Afrika ya kusini kununua tena kiwanja kingine.

Baada ya Herbart kufa hakuna mtu yoyote anayemuhurumia Martha hasa wale nduguze Herbart. George ndugu yake na Herbart wanaongozana na wanakijiji wengine kuja kuchukua mali za Herbart kwani kimila mwanamke haruhusiwi kuridhi mali za mumewe na mbaya zaidi alikuwa kabila tofauti na Herbart. Lakini Martha anaonekana akikataa harakati hizo nakuwafukuza wanakijiji na George katika nyumba yake.

Kwa hivyo basi mvutano huu wa mila na desturi za zamani pamoja na usasa ambao unaonekana katika tamthilia hii ndio ukamfanya mwandishi aite tamthilia hii kwenye ukingo wa thim.

Kwa hivyo basi kwa mujibu ya mifano hii ni dhahiri kwamba tamthilia ya kwenye ukingo wa thim inalenga kumulika hali ya mvutano baina ya mila na desturi za kale na usasa katika jamii aliyoiwakilisha.

Katika tamthilia hii mvutano unaojitokeza na vyanzo mahususi vinavyousababisha ni vilevile katika jamii ya Wachaga mkoani Moshi, mvutano huu huwa na vyanzo vyake vyanzo hivi ni sambamba na vyakwenye tamthilia kwani tamthilia ni tanzu ya fasihi ambayo ni kioo cha jamii.

Kulingana na mwana philosophia Jannet M. Scott (2002) " mila imejichanganya sana na utamaduni wa leo ndomaana kuna migogoro"

1.2 Swala la utafiti

kuna swala tata la mvutano baina ya mila za zamani na usasa uliopo katika maisha ya jamii ya Wachaga mkoani Moshi . kwahivyo mtafiti aliibua moyo na hamu yakuchunguza ikiwa ndivyo ilivyo katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na kuchunguza vyanzo na sababu zakutokea kwa mvutano huu baina ya mila za kale na usasa mkoani Moshi pamoja na mbinu za kurekebisha hali ya kimaisha hii katika jamii ya Wachaga mkoani Moshi.

Tamthilia ya kwenye ukingo wa thim ni kazi ya kubuni lakini mtafiti ameilinganisha na maisha halisi kwani fasihi ni kioo cha jamii. Yaani mtafiti alichunguza mvutano baina ya mila za zamani na usasa ya kwenye tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na mvutano wa mila na usasa katika jamii ya wachaga mkoani moshi.

1.3 Madhumuni ya utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kulinganisha mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika jamii ya tamthiliani na jamii ya Wachaga mkoani Moshi.

1.4 Malengo mahususi ni;

Kubaini hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kweye ukingo wa thim na mvutano wa mila za zamani na usasa ule uliojitokeza katika jamii ya Wachaga

- Kueleza vyanzo vya mvutano wa mila za zamani na usasa kama unavyojitokeza katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na mvutano wa mila na usasa unaojitokeza katika jamii ya Wachaga.
- Kubainisha uhusiano kati ya hali hizi mbili yaani mvutano baina ya mila za zamani na usasa kwaajili ya kupata ukweli dhabiti.
- Kupendekeza mbinu za kukomesha hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa ili matatizo yanayowakumba wananchi wa mkoa wa Moshi kama kutengwa na familia zao kisa wameenda kinyume na mila za jamii yao,kuvunjika kwa uchumba na hata ndoa za wapendanao viweze kukoma.

1.5 Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu unamsaidia mtafiti mwenyewe kwani unatimiza baadhi ya mahitaji ya kuitimu kwa shahada ya sanaa na elimu ya chuo kikuu cha Kampala International University.

Pili, kwa kuwa hakuna utafiti uliowahi kufanywa juu ya uchunguzi linganishi wa mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika jamii ya wachaga mkoani Moshi hivyo itasaidia kutatua mvutano huu.

Utafiti huu unalenga kuhimiza mbinu za kurekebisha hali ya maisha iliyomo mkoani Moshi,kwa hivyo mapendekezo kulingana na wahojiwa yatarejelewa kwa mujibu wa kurekebisha hali hii.

Uchunguzi huu utakuwa kumbukumbu kwa idara ya lugha na mawasiliano ya chuo kikuu cha Kapala International University na utatumiwa kama marejeleo.

1.6 upeo wa utafiti

Utafiti huu ulikuwa na upeo wa kiufundi, upeo wa kijografia na upeo wakiwakati.

1.6.1 Upeo wa kiufundi

Upeo huu ulilenga kuchunguza mvutano wa mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ule unaojitokeza katika jamii ya Wachaga mkoani Moshi ili kupendekeza mbinu mwafaka za kurekebisha hali hii yakimaisha.

1.6.2 Upeo wa kijografia

Uchunguzi huu ulifanyiwa katika vijiji vya kibororoni, mwika, kibosho na sambarai. Vijiji hivi ndivyo vilivyotumiwa ili kukusanya data ya utafiti huu. Mtafiti alitumia vijiji vine tu kwasababu ya upungufu wa vifaa na pesa ya kutumia katika vijiji vingi.

1.6.3 Upeo wa kiwakati

Utafiti ulifanywa kwa muda wa miezi mitano yaani kuanzia mwezi wa nne hadi mwanzoni mwa mwezi wa nane. Mda huu ulimsaidia mtafiti kukusanya data iliyohusu mada ya utafiti wake.

1.7 Shida zilizomkumba mtafiti

Mtafiti alikubwa na shida ya hela za kuendesha uchunguzi wake. Hata hivyo ilimbidi mtafiti kupanga bajeti yake kwa ajili ya kulenga mambo muhimu tu.

Isitoshe mtafiti alikumbana na shida ya kutoaminiwa na wahojiwa, yaani kuchukuliwa kama mpelelezi jambo ambalo lilizuia baadhi ya wahojiwa kumpokea vilivyo, ilimbidi mtafiti kutoa kitambulisho chake cha Chuo Kikuu cha Kampala International University ili kudhihirisha kuwa ni mwanafunzi.

Hali kadhalika mtafiti alikubwa na shida yakutokuwa na muda wa kutosha ili kuzingatia kazi yake vikamilifu. Kwaiyo mtafiti alitumia vipindi alivyokuwa huru wakati wake chuoni.

Mtafiti alipata shida ya uchapishaji maana huchukua muda mwingi pamoja na hela nyingi. Hata hivyo shida hii ilitatuliwa na mtafiti kutumia ujuzi wake wa tarakilishi kwa ajili ya kukwepa pesa za uchapishaji.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.0 Utangulizi

Sura hii inahusu yaliyoandikwa na yenye uhusiano na mada ya utafiti. Katika sura hii mtafiti alizingatia mada ya utafiti kwa kulinganisha na mapitio yenye uhusiano ili kuchunguza mvutano kati ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na hali hiyo mkoani Moshi.

Katika sura hii mtafiti huchunguza mada kifinyu finyu ila tu atazingatia pia maoni ya wataalam mbalimbali pamoja na tafiti mbalimbali zenye uhusiano na mada yake, mtafiti pia alichunguza vitabu mbalimbali vinavyozunguzia kuhusu mvutano baina ya mila za zamani na usasa, kwa mjibu wa mtafiti itakuwa bora kuangalia upya kazi za utafiti kwa ajili ya ulinganishaji mzuri na kwa uzuri wa kazi yake.

2.1 Maandishi kuhusu mila na usasa

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili sanifu ,istilahi uchanganuzi hufasiliwa kama uelewaji wa dhana, fikra au maandishi ya mtu. Pia uchunguzi ni kufahmu daima kuhusu hali mahususi nayajumla katika haki za binadamu.

Kwa hivyo kulingana na fasihi kamili ya isilahi hii katika kamusi ya Kiswahili sanifu, ni dhahiri kwamba katika uchunguzi huu mtafiti alichunguza, alichambua na kufafanua kwa kina dhana ya mvutano wa kimila na kisasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na hali hiyo kayika jamii ya Wachaga.

Mila hii ni miiko, taratibu au sheria zilizowekwa na wazee wetu wa zamani kwa zumuni la kufwata katika jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Kulingana na Wikipedia (2014) wanatafsiri neno utamaduni kama "jinsi binadamu anavyokabili maisha katika mazingira yake kama ujuzi, imani, sanaa, maadili sheria, desturi ambavyo mtu anajipatia kama mwanajamii"

Usasa pia hii ni hali yakufwata mila na desturi za watu wa nje haswa wazungu kwa kuiga limi zao,mavazi yao na hata tamaduni zao.

Kulingana na mwandishi S.A.Mohammed (2013) " usasa ni kuigiza kama wazungu kwa kufuata mila zao"

Kwa mfano Herbart aliweza kumuoa bi Martha ambaye walikuwa wanatoka makabila tofauti hali hiyo ilileta mvutano, " ndiyo kweli wenyewe siku hizi mambo ya kisasa kila kitu cha kisasa mtazame Herbart na Martha , Herbart hii yakuoa kabila moja imekwisha....."

2.2 Maandishi kuhusu jamii

Jamii ni mkusanyio wa watu wenye kuishi pamoja katika eneo moja la kijografia wakiunganishwa na historia. Jamii hutambuliwa kwa utamaduni wao, lugha, mila na desturi.

Kwa mfano, makabila mbalimbali huwa na miundo yao wenyewe ya kujitawala na namna wanavyofanya shughuli zao za kiuchumi kama vile wafugaji au wavuvi, mafunzo na taaluma, mfano jamii ya Wachaga mkoani Moshi.

Kwahivyo ili eneo liwe jamii lazima yafuatayo yawepo

- Watu wa jinsia zote pamoja na rika zote yaani wanawake kwa wanaume, wazee kwa vijana.
- Wanaoishi pamoja kwa mfano wakazi wa vijiji vya kiborororoni, mwika, kibosho na sambarai.
- Ndani ya mipaka ya kieneo kwa muda Fulani unaoweza kuwaunganisha kama wale wakazi wa Moshi.
- Lugha inayowatambulisha kwa mfano ya kichaga kwa wakazi wa mkoa wa Moshi
- Utaratibu maalum wa kushiriki mila za mitambiko haswa mwishoni mwa mwaka.

Kwa kuzingatia mahitaji ya eneo kuitwa jamii, mkoa wa Moshi ni jamii kamili kwa sababu hutosheleza maitaji yote ya jamii kulingana na mtaalam Reis na Rusbult (2004).

2.2.1 Maandishi kuhusu jamii ya Wachaga

Moshi ni mkoa unaopatikana Mashariki mwa Tanzania. Wengi wa wakazi wa jamii hii ni wachaga wakichanganyikana na wapare ambao kabila la wapera wengi wao hukaa kwenye vimilima vya moshi, lakini idadi yao ikiwa ndogo kabisa kulinganisha na wachaga waishio Moshi. Kabila kubwa na lawatu wengi waishio Moshi huitwa chagga au wachaga, ingawa

wachaga hawa wamegawanyika katika makundi mbalimbali kama ;Wamachame, Wakibosho, Wakishimundu, Wamarangu, Warombo, Wasiha na Wahuru. Mkoa huu unawakazi wengi zaidi ya watu (185,000) kulingana na sensa ya mwaka (2012). Kiuchumi wakazi wa Moshi ni walimaji kwa kiasi kikubwa kuliko wafugaji. Biashara ni mojawapo ya shughuli kubwa inayofanyika mkoani Moshi. wanajamii wengi wa mkoa huu hawapendi sana elimu ila hujikita sana katika biashara maana huamini elimu hupoteza muda.

Jamii hii ni maarufu sana kutokana na tabia yao yakupenda sana hela na ujishuhulishajiwao katika maendeleo kutokana na idadi yao kuwa kubwa katika biashara mbalimbali nchini Tanzania. Moshi pia ni mkoa wa kitalii na wenye kivutio cha kitalii yaani kuwepo kwake kwa mlima Kilimanjaro ambao ndio mlima mrefu Afrika.

Kwa kuzingatia vijinji vya utafiti, kibororoni, mwika, kibosho na sambarai ni vijiji vinavyopatikana mkoani Moshi.vijiji hivi vina idadi ya watu elfu nne na nane (4008). Hawa hujumuisha wanawake, wanaume pamoja na watoto. Maisha vijijini humo niyakawaida yani kuna familia, ufanyaji wa kazi mbalimbali, biashara na familia. Kwahiyo hivyo ni vijiji kama vingine hali ya mvutano wa kimila na usasa hujitokeza.

2.3 Maandishi kuhusu fasihi

Fasihi hutokana na neno la kiarabu lenye maana "tawi". Yaani ni utanzu wa sanaa ambao hutumia lugha ya mazungumzo au maandishi ili kufikisha, kuwasilisha ujumbe kwa hadhira husika.

Waaataalamu wengi wamelielezea neno hili fasihi kwa hivyo ufafanuzi na nadharia juu yake ni nyingi. Hata hivyo wengi wao wote wamehusika na fasihi kwa ujumla au katika fasihi maandishi katika jitiada zao zote za kufafanua na kuelezea taaluma ya fasihi, kuna misingi kadhaa ambayo wengi wao huikubali au wasingepinga kama imewekwa wazi zaidi.

Ukiitazama fasihi kwa umbo lake la nje na umbo lake la ndani utaona kuwa ni taaluma iliyojengwa na maneno, maneno yenyewe hutumia fani maalum za aina mbalimbali kutolea makusudi au maudhui ambayo humzingatia binadamu maishani. Kama vile mshitakiwa awezvyo kutoka katika hatia japo awe mkosaji kwa kutumia ufundi wa maneno, nakama vile awezavyo kuingia hatiani na kuadhibiwa iwapo awe sio mkosa kwa utumiaji wamaneno hivyo hivyo. Kufanikiwa au kutofanikiwa kwa fasihi umo katika utumiaji wa maneno.

Kwa hitimisho utumiaji wa kazi ya fasihi na hali halisi imejaa ndiyo maana mtafiti akalinganisha hali ya tamthiliani na ile ya Mkoani Moshi.

Hii ni kwasabu zilizoelezwa kwamba fasihi hutumia tu maneno lakini ni kiwakilisho cha jamii Fulani aidha mtafiti alilinganisha vijiji tamthiliani na vijiji mkoani Moshi.

2.4 Maandishi kuhusu mada

Mtafiti alisoma kazi mbalimbali za wataalamu tofauti na kugundua maandishi yenye uhusiano na mada ya utafiti. Maandishi haya ni kama yafuatavyo;

Kulingana na Ludovik Joseph (2003), "dunia imebadilika kutokana na teknolojia,staili mpya na mbinu za kisasa katika uchunguzi bila kusahau maisha ya kila siku,lakini bado kuna mvutano wa nguvu kati ya mila na usasa"

Ingawa teknolojia na utamaduni wa kigeni umekidhiri sana katika jamii zetu lakini bado tunaona ni jinsi gani bado kuna jamii au kikundi cha watu kinachoamini bado mila zetu za zamani zinaumuhimu na ninzuri kuliko usasa.

Kwa kuzingatia utafiti wake Winson Churchill (1996) "pasipo na mila ni sawa na kundi la kondoo bila mchungaji na pasipo usasa ni sawa na toroli bila mwendeshaji"

Huu ni mvutano dhahiri ila tunapaswa kujua kila kitu kinategemeana na kingine yaani kusingekuwepo na mila tusingeweza kuujenga usasa na pia mila zisingeweza kukumbukwa bila kuwepo kwa usasa,

Kwa mujibu wa Mahatma Gandhi (2001), Tamaduni za mataifa mbalimbali zimesambaratika kutokana na usasa uliojitokeza ingawa mila za watu zimo ndani ya mioyo yao ila akili zao zinajifanananisha na miiko yawengine".

Mila bado zipo miongoni mwa wanajamii wengi ingawa mila hizi zinavutana na usasa kwani mila hukaa kwenye mioyo ya watu ingawa macho na akili huvutiwa na mambo yanavyotendeka haswa katika utandawazi na uhuru ambayo mambo mengi yakisasa hutupatia.

Kulingana na Antonio Gramson (2003), " Matatizo mengi yanayojitokeza katika mambo ya kisasa husababishwa sana na desturi na mila zetu kwani huleta kuishi pasipo na imani na imani haba huleta kutoweka kwa uhuru".

Uhuru wa maisha hutoweka pale ambapo mtu hupoteza imani ya maisha hasa wakati anaposhindwa aangukie sehemu gani ya maisha yaani afwate kanuni za mila zinavyomwambia au afwate kanuni za kisasa jinsi zinavyomuelekeza, hivyo basi huleta mvutano mkubwa baina ya hivi vitu viwili.

Katika kitabu cha "Maisha na mila" kilichoandikwa na Jose Andrew Pilenta (1995) alisema kuwa "mila ni idadi ya mambo yaliyotokea hapo kale na usasa ni mpangilio wa maisha ya mtu au jamii Fulani"

Kulingana na kitabu hiki tunaona mila nyingi zilitokana na mambo mbalimbali yaliyokuwa yakitendeka hapo zamani, na kutokana na mambo hayo ikawa haina budi kuweka mipaka au kanuni mbalimbali ambazo kanuni au mipaka hiyo ndiyo waliita mila. Lakini kwa hali ya sasa hivi kwa kiasi Fulani mbayo yaliyokuwa yanatendeka zamani hayapo tena hivyo basi hakuna budi kufwata kanuni na mipaka iliyowekwa katika kare hii ili kuendana na watu wengine duniani.

Kulingana na utafiti uliofanya na Dr Lairry Dossey (2010), mwana saikolojia na mtaalamu wa mambo ya ndoa na familia alibaini kuwa wapenzi wengi haswa wa dini tofauti wanashindwa kuoana kutokana na watu hao kuwa na utafauti katika mila na hata itikadi yao, jambo hili huchangia baadhi yao kutengwa kwani hujiamulia kufwata matakwa ya mioyo yao kwa kuwa pamoja bila idhini ya wazazi ingawa wengine huishia kujiua au kutoroka majumbani kwao kwa kukataliwa kuwa na wapenzi wawapendao. Aliishia kusema kuwa " utamaduni wa watu wengi huwa ni kifungo katika jela ya kisasa".

Matokeo ya utafiti huu unaungana na habari moja iliyotekea mkoani Moshi katika kituo cha redio cha Moshi mjini kuwa jamaa mmoja atokaye kijiji cha Mwika alikutwa kafariki baada ya kupigwa kipigo cha mbwa mwitu na vijana wa kiarabu ambao hawakufahamika kwa majina, lakini chanzo hiki kilitokana na kijana huyo kuonywa mara nyingi kuacha mahusiano na mtoto wa kiarabu wa mfanyabiashara mmoja maarufu wilayani hayo kwani kijana huyo hakuwa wa asili hiyo, baba wa binti alipokuwa anahojiwa kuhusiana na tukio alinukuliwa akisema kuwa"ingawa utamaduni wetu hauruhusu ila mambo ya kisasa yamemuangamiza huyu kijana".

Kwa mujibu wa Theodore Bikel(2015) "hatutakiwi kuwa na usasa ili uishi leo, kwa ujumla maitaji ya binadamu yanaitaji maitaji ya usasa pamoja na miundo ya mila ili uishi leo"

Ni jinsi gani vitu hivi vinavutana lakini vyote vinaumuhimu katika maisha yetu maana mtu hawezi ishi bila usasa na mila pia humwongoza mtu na kumfanya aishi kimaadili

Tukiangalia kitabu cha Romio na Juliet kilichoandikwa na Sheksphere tunamwona baba yake Juliet bwana Capulet akimwambia bintie lazima aolewe na Paris ingawa Juliet alikuwa akimpenda Romio, hivyo basi Juliet alinukuliwa akiwa anamwambia Nesi wake kuwa " mila na tamaduni za familia yangu zinanifanya nisiwe na mtu nimpendae ila kwa hali ya sasa sidhani kama nitafwata matwaka yao"

Kwa kuzingatia utafiti wake Jiddu Kishramit (1996) " utamaduni ulikuwa ulinzi wetu ila kutokana na usasa akili zetu zimefunikwa na mambo mapya nakutufanya tufe na kupotea"

Ingawa mambo mengi ya kisasa yameonekana yakifungua ubongo na fikra zetu pia kurahisisha maisha yetu lakini yamekuwa na changamoto kubwa nakutufanya tuzidi kuangamia na kusahau mila zetu ambazo ndizo zilikuwa muongozo wetu.

Kulingana na utafiti uliofanywa na Arjana Begzati pamoja na Maddy Vogel (2014)kuonyesha sababu zinazofanya kuwepo kwa tofauti baina ya usasa na mila kama zifuatavyo;

- **Ubadilikaji wa tabia**; hapo zamani watu hawakuwa na uhuru wa kufanya mambo kama wanavyotaka lakini kila kitu kilikuwa nilazima kifanyike chinin ya muongozo wa wazee amabo wao ndowalikuwa waamuzi wa kila jambo hata katika mambo bonafsi ya mtu. Tukiangalia katika hali ya usasa kila kitu kinafanywa kwa uhuru yaani mtu anakuwa na maamuzi ya kujiamulia jambo ambalo anataka lifanyike bila ushirikiano wa wazazi au wazee wanaomzunguka.
- **Dhana ya ndoa kama upendo**, hisia, mapenzi, mahaba na kujali; dhana hii ilikuwa yakuheshimiwa sana kwani msichana alikuwa akitafutiwa mume wa kumuoa na wazazi wake na mwanaume pale alipompenda msichana alikuwa hamwambii bali huwaambia wazazi wake na wazazi huwafwata wazazi wa msichana. Kwa sasa imekuwa tofauti kwani hisia za msichana na mvulana na makubaliano yao ndio huwafanya wapendane na hata kufikia kuoana.
- **Mavazi;** kutokana na mila za zamani wanawake walikuwa wanavaa mavazi yakufunika miili yao haswa sehemu za siri kama matiti, vifua, mapaja na makalio, lakini kutokana na usasa wa sasa hali hii imebadilika kwani vijana wengi huvaa mavazi ya kuacha miili yao wazi.

- **Mabadiliko ya lugha**; hapo zamani wanajamii walikuwa wakiongea lugha mama zao nahata watoto walikuwa wakifunzwa kwa kutukia lugha hizi, lakini mambo yamekuja badilika pale ambapo watu wengi hawajui lugha mama zao lakininwanajua kiingereza na shuleni pia lugha ya mawasiliano inayotumika ni kiingereza.
- **Imani na dini**; mila za watu zilikuwa kwenye vitu, miti na milimani sehemu hizi zilitumiwa kama mahali pa ibada na watu walikuwa wakimuomba miungu yao kupiyia sehemu hizi, hawakuwa na maandishi nyoyote yale ila walifata imani yao nakuamini tu Mungu yupo, lakini sasa kumekuwa na dini mbalimbali kama wakristo, waislamu, wapagani, wayunani, wahindu nanyinginezo ambazo hufanyika misikitini ama makanisani.

2.5 Hitimisho

Katika hitimisho kunakuwa na maandishi mengine mengi kuhusu mvutano wa mula na usasa katika kazi za fasihi na katika jamii halisi na mtafiti aliangaza kwa makini vitabu na makala kadhaa na kulinganisha maandishi haya na data aliyoipata uwanjani,na bila shaka mtafiti alilinganisha kijiji cha riwayani na vijiji vya Moshi.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alishughulikia mbinu alizotumia katika kukufanya data pamoja na uchanganuzi wake.mbinu hizi nikama vile hojaji, mahojiano na uchunguzi shirikishi.

Aidha sura hii pia ilihusu uteuzi wa sampuli, uteuzi wa vifaa vya utafiti, utaratibu wa utafiti na hatimaye uchanganuzi wa data.

3.1 Utaratibu wa utafiti

Mtafiti alianza uchunguzi wake kwa kutayarisha maswali ya hojaji ambayo yaliyojazwa na wajibu wake.

Aidha mtafiti alijitambulisha kwa wahojiwa wake kama mwanafunzi wa chuo kikuu cha Kampala International University. Aliwatambulishia shughuli nakuwapatia hojaji, wahijiwa walijibu maswali ya hojaji na kumrudishia mtafiti.

3.2 Uteuzi wa sampuli

Mtafiti aliteuwa vijiji vinne kuwakilisha mkoa mzima wa Moshi na vijiji hivi vilikuwa Kibororoni, Mweka, Kibosho, na Sambarai. Vile haingewezekana kuhoji kila mtu katika vijiji hivi, mtafiti alitumia sampuli huru kuchagua wahojiwa wake. Mtafiti alitangulia kwa wakuu wa kila kijiji na kumwarifu juu ya shughuli zake za utafiti. Wakuu wa vijiji ndio waliomwelekeza kwa wazee, wanawake na vijana ambao walimpatia ujumbe mtafiti. Mtafiti aliwapendelea wazee kwani ndio wenye tajriba kimaisha. Vijana pia walifaa kwani ndio mara nyingi hupata changamoto dhidi ya mambo ya kisasa na mila inavyoongea, shughuli ya kutafuta wahojiwa ilifaulu na hojaji zikapewa wahojiwa.

3.3 Mbinu za kukusanya data

Mtafiti alitumia hojaji, mahojianao pamoja na mbinu shirikishi ili kupata data iliyokusudiwa. Mbinu hizi zilimsaidia mtafiti kupata data iliyofanikisha uchunguzi wake.

3.4 Hojaji

Mtafiti aliandika maswali katika karatasi yake na kuwapa, wajibu wake ili kupata taarifa iliyofanikisha utafiti wake. Maswali haya katika hojaji hii yalihusu vipengele maalum vya mvutano baina ya mila na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na jamii ya

Wachaga mkoani Moshi. Mtafiti alitumia mbinu hii kwakuwa wahojiwa wake kwa bahati nzuri walijua kusoma na kuandika.

3.5 Mahojiano

Mtafiti alitayarisha muongozo wa mahojiano, mtafiti alipendekeza kuhoji wahojiwa ambao walikuwa na ujuzi wa mvutano baina ya usasa na mila kwa kuwauliza kwanza ikiwa wana ujuzi kiasi. Mahojiano haya yalimsaidia mtafiti kupata taarifa ambayo huenda ingekuwa vigumu kuipata kwa kutumia hojaji na mbinu nyingine.

3.6 Uchunguzi shirikishi

Hii ni mbinu ambapo mtafiti alijishughulisha na kushirikiana na wahojiwa wake na kuwazoea akiwa na lengo la kupata data kamili kutoka kwao vilivyo.

Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kwa kusikiliza nyimbo anuani za Kichaga ili aweze kubaini ni jinsi gani wanachukulia mvutano wa mila na usasa unavyojitokeza katika jamii ya Moshi na katika tamthilia ya utafiti. Mtafiti alipendelea kusikiliza nyimbo, methali, misemo, majina ya Wachaga kwani husawili hali maishani mwa wakazi ya jamii husika. Wahojiwa kadhaa waliimba nyimbo zinazo sawili mvutano baina ya mila na usasa hasa katika jamii yao. Haya yalifanyika katika kijiji cha Mwika.

3.7 Uteuzi wa vifaa

Mtafiti alitumia vifaa kama kamera ya kunasa video na sauti za wahojiwa, hojaji na madaftari ya kuweka rekodi za kumbukumbu kutoka uwanjani, vifaa hivi vilimsaidia mtafiti kukusanya data iliyofanikisha utafiti wake.

3.8 Uchanganuzi wa data

Mtafiti baada ya kukusanya data aliitafsiri na kuichanganua na kuitathimini na hatimaye akalinganisha maswali ya utafiti wake ili kupata ushaidi wa kudhibitisha au kukanushia maswali ya utafiti wake. Mkabala wa kuthaminio ulitumiwa kuchanganua data iliyokusanywa uwanjani.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.0 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchanganuzi wa kina wa data iliyokusanywa kuhusu uchanganuzi linganishi wa mvutano wa ukale wa kitamaduni na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ule unaojitokeza katika jamii ya Wachaga Mkoani Moshi.

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kutathmini majibu ya hojajai, mahojiano na uchanganuzi shirikishi ili kumsaidia mtafiti kugundua uzito wa data kama ushahidi wa kudhibitisha au kukanushia maswali ya utafiti wake. Majibu yaliwakilisha kulingana na malengo ya utafiti.

Vichwa kadhaa vilitumiwa kukusanya data kama vifuatavyo;

Umri wa wajibu, usikilizaji wa nyimbo za kisasa za kichaga. Taswira ya hali katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim, vyanzo vya mvutano baina ya ukale wa zamani na usasa tamthiliani, vyanzo vya mvutano wa mila za zamani na usasa mkoani Moshi na usomaji wa kazi tofauti kama marejeleo kwa mujibu wa kukamilisha lengo la mtafiti.

4.1 Uwasilishaji na uchanganuzi wa data

Katika uchunguzi huu mtafiti alitumia jumla ya wahojiwa hamsini (40). Wakati wa utathimini mtafiti alitumia herufi (K) kuwakilisha kijiji cha Kibororoni, (KB) kuwakilisha kijiji cha Kibosho (M) kuwakilisha kijiji cha Mwika, na (S) kuwakilisha kijiji cha Sambarai.

Njia ya kithamano ilitumika katika kuchanganua data iliyokusanywa uwanjani, uchanganuzi huu ulizingatia madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti na ulinganishaji wa mvutano baina ya ukale na usasa tamthiliani na ule mkoani Moshi.

4.2 Tathmini ya hojaji na mahojiano

Mtafiti aliwapa hojaji wahojiwa kumi kutoka kila kijiji. Mtafiti alikuwa na lengo la kupata habari kuhusu usawari wa hali kamili ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ile hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika mkoa wa Moshi.

Wahojiwa walipoulizwa kutaja jinsia zao majibu yao yalikuwa;

Jedwali 4:1 jinsia ya wahojiwa

Kijiji	Kiume	Kike
K	05	07
KB	05	06
M	06	07
S	07	08
Jumla	22	28
Asilimia	44	56

Matokeo ya uwanjani yalionyesha kuwa;

Wahojiwa ishirini na wawili yaani asilimia (44%) walikuwa wanaume na wahojiwa ishirini na wanane yaani asilimia (56%) walikuwa wanawake.

Pia wahojiwa waliulizwa kudhihirisha umri wao na majibu yao yalikuwa kama yafuatavyo;

Jedwali 4:2 umri wa wahojiwa

Kijiji	(15-24)	(25-35)	(35-zaidi)
K	04	06	O4
KB	04	O5	O4
M	02	O8	02
S	03	O5	03
Jumla	13	24	13
Asilimia	26	48	26

Kulingana na matokeo yaliyotokea uwanjani, wajibu kumi na tatu yaani asilimia ishirini na sita (26%) walikuwa na umri wa miaka kati ya kumi na tano na miaka ishirini na mine, wahojiwa ishirini na wane (48%) walikuwa kati ya miaka ishirini na mitano na miaka thelathini na mine na hatimaye wajibu kumi na watatu yaani asilimia ishirini na sita (26%) walikuwa na miaka thelathini na mitano na zaidi.

Isitoshe wahojiwa walipoulizwa ikiwa wanaujuzi na tajriba ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa walijibu ifuatavto;

Jedwali 4:3 je unaujuzi na tajriba ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa mkoani humu Moshi?

KIJIJI	NDIO	HAPANA	KIASI KIDOGO
K	9	1	3
KB	8	0	5
M	7	0	3
S	9	0	6
JUMLA	32	2	17
ASILIMIA	64	2	34

Kulingana na matokeo ya uwanjani, wahojiwa thelathini na wawili (64%) walisema kuwa walishawahi kusikia hali ya mvutano baina ya mila na usasa pamoja na kushughulika katika hali kama hiyo, mhojiwa mmoja (2%) alijibu kuwa hajawahi na kumi na saba (34%) walisema kwamba wamezisikia hali hizo na kushughulika kwa kiasi kidogo.

Aidha mtafiti alipowahoji wahojiwa wake kuhusu aina za mvutano wa mila za zamani na usasa walijibu haya.

Jedwali 4:4 aina za mvutano baina ya mila za zamani na usasa mkoani Moshi;

Kijiji	kimapenzi	Kifamilia	kisiasa	kibiashara
K	6	4	3	2
KB	4	2	3	3
S	5	2	4	0
M	5	1	1	3
Jumla	20	10	12	8
Idadi	40	20	24	16

Kwa hivyo kulingana na matokeo ya uwanja, wahojiwa arobaini (60%) walitaja mvutano baina ya mila za zamani na usasa ni wakimapenzi, wahojiwa kumi (20%) walisema mvutano baina ya mila za zamani na usasa ni wakifamilia na kumi na wawili (24%) walisema mvutano wa mila na usasa ni wakisiasa na wahojiwa nane (16%) wakajibu kwamba umvutano baina ya mila za zamani na usasa ni wa kibiashara.

Aidha waliojibu mvutano wa kimila na usasa ni wakimapenzi walisisitiza kwamba ndio uliozidi kabisa.

Hali kadhalika wahojiwa walipoulizwa endapo tamthilia ya kwenye ukingo wa thim inasawiri hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa mkoani mwao walijibu ifuaatavyo;

Jedwali 4:5 mvutano wa mila na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim

Kijiji	Ndio	Hapana	Kiasi kidogo
K	10	0	6
KB	8	1	4
M	9	1	3
S	7	0	2
Jumla	34	2	14
Asilimia	68	4	28

Kwa mujibu wa data iliyokusanywa uwanjani wahojiwa thelathini na wanne (68%) walisema ya kwamba tamthilia ya kwenye ukingo wa thim inasawiri hali mbalimbali za mvutano baina ya mila za zamani na usasa . isipokuwa wawili (04%) waliojibu hapana, wahojiwa wawili walipoulizwa kwanini walikana walijibu ya kwamba hawakuwa na ujuzi wowote juu ya tamthilia hii . wahojiwa kumi na nane (28%) walijibu kiasi kidogo.

Fauka na hayo mtafiti alipowauliza juu ya vyanzo vya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na na katika jamii yao walisema ya kwamba nyanzo ni vingi sana ila tu vyote husababishwa na ubinadamu, yaani binadamu popote pale apatikanapo huwa lazima kutokee mvutano baina ya umila na usasa

Isitoshe mtafiti alipowauliza wahojiwa wake ikiwa majina, nyimbo na methali vina sawili nmvutano baina ya mila za zamani na usasa walijibu kama ifuatavyo;

4:6 Je majina na methali za kichaga husawili hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa?

Kijiji	Ndio	Hapana	Kiasi kidogo
K	10	1	2
KB	9	0	3
M	9	0	4
S	8	0	4
Jumla	36	1	13
Asilimia	72	2	26

Matokeo ya uwanjani yalidhihirisha kuwa asilimia sabini na mbili (72%) ya wahojiwa walijibu kwamba majina ya kichaga pamoja na methali zina dhima kubwa katika jamii yao haswa hasa kusawili hali ya maisha kama mvutano baina ya mila za zamani na usasa.

Kadhalika wahojiwa waliohusishwa katika utafiti huu walipoulizwa nyimbo, majina na methali zenye ujumbe wa kimvutano wa mila za zamani na usasa walisema zipo na walitaja kadha wa kadha.

Majina haya ni kama vile Namte, Loishiye, Namnyaki, Shogongo, Kingunge, Alinaninye. Kwa upande wa misemo walitaja kama vile; Eembe nenshisha , Nanshakulanyiro emberoo. Hata hivyo kwa upande wa nyimbo walitaja zifuatazo; Nikusaidiaje- Professor J, Sizonje- Mrisho mpoto na Banana zoro, Twende tukatambike mizimu- Wannne star.

4.3 Majadiliano ya matokeo

Matokeo ya utafiti yamejadiliwa kulingana na malengo ya utafiti,

Malengo ya utafiti huu yalikuwa kulinganisha vyanzo vya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ule Mkoani Moshi, kuchunguza mbinu mwafaka za kutatua shida hii.

4.3.1 Lengo la kwanza

Kuchunguza vyanzo vya mvutano baina ya mila za zamani na usasa tamthiliani na Mkoani Moshi

Vyanzo vya mvutano baina ya mila za zamani na usasa kulingana na wahojiwa ni kama vifuatavyo;

Ubadilikaji wa tabia haswa kwa wakazi wa Mkoa wa Moshi.ubadilikanaji huu umeletwa kutokana na hali ya utandawazi na watalii wengi wanatembelea Mkoa wa Moshi kutokana na kivutio cha mlima Kilimanjaro,hapo zamani watu wa mkoani Moshi hawakuwa na uhuru wa kufanya mambo kama wanavyotaka kwani kila kitu kilikuwa ni lazima kifanyike chini ya muongozo wa wazee wa mila ambao ndio walikuwa waamuzi wa kila jambo hata katika mambo binafsi ya mtu. Lakini hali hii imebadilika na kusababisha mvutano mkubwa kati ya umila na usasa kwani kila kitu kinafanywa kwa uhuru yaani mtu anakuwa na maamuzi ya kujiamulia jambo analotaka lifanyike bila ushirikiano wa wazazi au wazee wanaomzunguka.

Mhojiwa aliyehojiwa alisema kuwa dhana ya mahusiano kama ndoa, upendo, hisia na mapenzi imeleta mvutano mkubwa baina ya mila za zamani na usasa kwani hapo zamani msichana alikuwa akitafutiwa mwezi wa maisha na wazazi wake na mwanaume pia inapotokea amempenda msichana alikuwa akiwaambia wazazi wake na wao ndio waliokuwa wakipeleka ujumbe huo kwa wazazi wa msichana. Mhojiwa aliendelea kueleza kwamba mila za kichaga zilikuwa haziruhusu msichana kuolewa kama hayuko bikira kwani usiku kabda ya harusi yao msichana na mvulana walikuwa wanakutanishwa na kufanya mapenzi ili kuhakikisha kama msichana bado ni bikira na kama msichana akikutwa sio bikira ndoa hiyo ilivunjwa mara moja na msichana alikuwa wa kutengwa na jamii. Mhojiwa alisema kwamba hali hiyo haiangaliwi kwa sasa kutokana na utandawazi mwingi hivyo kuacha mvutanao baina ya usasa na mila za zamani kuwa mkubwa zaidi kwani kuna familia ambazo bado wanaenzi mila za zamani.tukilinganisha na hali ya tamthilia ya kwenye ukingo wa thim tunamwona Herbart aliyekuwa akipigwa vita kwa sababu alimuoa Martha ambaye hawakutoka katika kabila moja.

Sababu nyingine ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa kulingana na muhojiwa mwanamke ni kwamba "usasa ni mzuri kwani hali ya maisha yetu imeadilika hakuna haja ya kuficha mapenzi hasa kwa mwanaume umpendae ". Kulingana na jibu lake muhojiwa, " mimi naweza kumkumbatia na hata kumbusu mchumba wangu hadharani bila aibu yoyote hii inanifanya kuona mila za zamani zilikuwa zikitunyima mambo mengi sana"

Jibu la mwanamke huyo ni sawa na sababu ya vyanzo vya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim. Thibitisho ni pale Martha na Herbart wanapokuwa wanacheza mziki katika sherehe ya mtoto wao Cris huku wakiwa wamekumbatiana hali hii inamchukiza Stela na Lydia ambao wanaona kama wamevunja miiko ya mila zao kwa kucheza wakiwa wamekumbatiana mbele ya mtoto wao.

Mvutano wa mila za zamani na usasa hutokana na mabadiliko ya lugha. Mhojiwa kutoka katika kijiji cha Sambarai alinukuliwa akisema haya, hapo zamani wachaga wengi walikuwa wakiongea kichaga kama lugha mama yao na wachache wao wakichanganya na Kiswahili kama lugha ya mawasiliano kwa watu wa mikoa mingine lakini sasa zimezuka lugha nyingi kama kiingereza na kifaransa ambapo wakazi wengi hasa vijana wamekuwa wakizitumia lugha hizi hasa lugha ya kiingereza. Hali hii imewafanya vijana wengi kusahau lugha mama yao kwa kuenzi sana lugha za wazungu. Kwa kurejelea tamthilia ya kwenye ukingo wa thim tunamwona Cris akiwa anatumia sana kiingereza kwa sababu alisomea Amerika hivyo hakuwa na uwezo wa kuongea lugha mama yao na hata wazazi wake Martha na Herbart walikuwa wakiongea nae kwa kutumia kiingereza tu.

Mvutano baina ya mila za zamani na usasa husababishwa na imani na dini, kulingana na wahojiwa watano kutoka katika kijiji cha Kibosho na Mwika walisema kwamba mila za wachaga zilikuwa katika vitu kama milima na miti sehemu hizi zilitumiwa kama mahali pa ibada na watu walikuwa wakiiomba miungu yao kupitia sehemu hizi, waliweza kusadaka wanyama kama ngombe, mbuzi na kondoo kama njia moja wapo ya kuongea na miungu hiyo au kutoa shukrani. Lakini sasa watu wengi hawatambiki tena na kufanya ibada katika sehemu hizo kutokana na kuwepo kwa dini mbalimbali kama waislamu, wakristo na wapagani.wahojiwa waliendelea kuwa kuna familia nyingine bado wanaendelea mila hizi kama mwishoni mwa mwaka wachaga wengi ambao wanaishi mikoani ni lazima warudi Moshi ili kufanya mitambiko kama kutoa sadaka ya shukrani kwa miungu yao kwa sababu ya kuwalinda mwaka mzima katika mitambiko huyo hutumia pombe iitwayo Mbege pamoja na kuchinja wanyama kama mbuzi, ngombe na kondoo.

Kwa hitimisho mtafiti aligundua ya kwamba ingawa tamthilia ni kazi ya kubuni lakini inasawiri hali kamili ya kimaisha haswa mvutano baina ya mila za zamani na usasa. Hali hii nikwasababu ya vyanzo sawa katika jamii hizi zote.

4.3.2 Lengo la pili

Kueleza usawa katika hali ya mvutano wa kimila na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ule mkoani Moshi.

Matokeo ya kiutafiti yanaonyesha kuwa kuna usawa kati ya hali ya mvutano wa kimila na usasa tamthiliani na ile ya Mkoani Moshi. Kwanza kabisa kwasababu tamthilia ni utanzu wa fasihi. Fasihi kiufafanuzi ni kioo cha jamii na kwahiyo fasihi husawili yanayojitokeza katika jamii.

Kulingana na hali za mvutano wa mila za zamani na usasa kama vile; mvutano wa mila na usasa kimapenzi, kirafiki, kibiashara mifano hii yote hupatikana katika hali hizi mbili yaani hali ya mvutano wa kimila na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na hali hiyohiyo katika mkoa wa Moshi. Katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim tunamwona Herbart Aliyemuoa Martha ambaye niwakabila tofauti na yeye hivyo familia ya kina Herbart ikiwa kinyume na ndoa yao na hata kumchukia Martha. Katika hali hii tunaona usawa wa mvutano baina ya mila na usasa kuwa dhahiri

Kulingana na vyanzo mwafaka vya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika kitabu pamoja na mkoani Moshi, mtafiti aligundua kwamba tamthilia ya kwenye ukingo wa thim ni kiwakilishi mwafaka cha hali Mkoani Moshi. Mtafiti kulingana na wahojiwa wake mvutano baina ya mila na usasa husababishwa na mambo kadhaa kama vile; ubadilikanaji wa tabia, dhana ya mahusiano, mabadiliko ya lugha na imani na dini kama ilivyo katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim.

Hata hivyo mwisho wa hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa iligundulika kuwa ni sawa kama katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim ; katika data aliyopata mtafiti mwisho wa mvutano wa mila za zamani na usasa huwa vifo, mvutano zaidi, utengano na chuki mambo ambayo ndiyo mwisho wa hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim.

4.3.3 Lengo la tatu

Kuchunguza mbinu mwafaka za kutatua shida hii

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba kuna mbinu kadhaa zinazoweza kutumiwa katika utatuzi wa hali hii.

Mbinu hizi ni kama vile; kuwepo kwa maelewano kwa njia ya mazungumzo baina ya pande ote mbili yaani upande wa mila na upande wa usasa, kila pande yaani upande wa mila na upande wa usasa upate kuheshimiana kwa kugundua umuhimu wa uwepo wa pande zote hizo mbili, mipaka iwepo ili kulinda pande zote mbili na kutozileta ziingiliane.

Hitimisho

Katika uchunguzi uliofanywa na mtafiti ni dhahiri kuwa mvutano baina ya mila za zamani na usasa ni sumu kwasababu mvutano huu humfanya mtu anayepitia hali hiyo kutojiamini, kuishiwa na nguvu, kudharauliwa, utengano na hata kuufanya moyo kukata tama. Kwa hivyo

Ibrahim Hussein hakuandika jamii husika katika kitabu ila pia wakazi wa Moshi. Kwani mvutano baina ya mila za zamani na usasa umejaa pia.

Maudhui yanayoendeleza mvutano baina ya mila za zamani na usasa kwenye tamthilia ya kwenye ukingo wa thim ni kama vile ukombozi wa kiutamaduni, malezi, ndoa, elimu,migogoro,vifo, utengano ni katika maudhui haya ndipo mvutano baina ya mila za zamani na usasa ukadokezwa tamthiliani.

Ukombozi wa kiutamaduni

Katika kujadili udhui hili, mwandishi anaonyesha wazi kasoro zinazotokea katika utamaduni mwa Mwafrika. Utamaduni huu una athari mbaya kwa jamii kwani unasababisha mvutano mkubwa kati ya mila za zamani na usasa ambacho ndicho kiini kikubwa cha tamthilia ya kwenye ukingo wa thim. Ndoa ya Herbart na Martha ambao wanatokea katika makabila tofauti inavuruga utamaduni mila na desturi za Kiafrika ambao hauruhusu mtu kuoa au kuolewa nje ya kabila lake. Sababu hii inamfanya Lydia ukurasa wa 9 kusema kuwa " ndiyo kweli yenyewe siku hizi mambo ya kisasa kila kitu cha kisasa mtazame Herbart na Martha ,habari hii ya kuoa kabila moja imekwisha".

Malezi

Cris analelewa malezi ya kizungu zaidi kwani anasomeshwa Marekani na hata anaporudi nyumbani hafunzwi lugha mama yake wazai wake Martha na Herbart wanaendeleakukienzi kiingereza kuwa kukitumia hata arudipo nyumbani, ukiachilia hilo mbali Cris anamleta mchumba wake nyumbani nakuanza kulewa nae hata kuishia kucheza mziki hovyo jambo mbalo linamchukiza Stela kwani anaona kama nikuvunja miiko ya mila za kwao.

Ndoa

Ndoa ya Martha na Herbart haikubaliwi na wazazi wa Herbart kwani wanaona kama mwanao amevunja miiko ya mila zao kwa kuoa mwanamke ambaye hawajatoka kabila moja, hali hii inaenda upande wa Martha pia kwani wazazi wake wanamtenga kwa kumuona mtu asiyefaa katika jamii yao katika ukurasa wa 26-27 Martha anasema kuwa " jamii dangu jamaa moja walinitenga siku ya harusi yangu hata jamii ya mume wangu walimtenga pia siku hiyo...."

Migogoro

Kwanza kabisa kuna mgogoro baina ya Herbart na Palla na nduguze George kwasababu Herbart amepotoka kwa kuoa nje ya kabila lake. Pili, mgogoro unazuka baada ya kifo cha Herbart kati ya Martha na George pamoja na viongozi wa mila kwa upande wa Herbart kuhusu umiliki wa mali za Herbart kwani wanaamini kuwa mwanamke kutokana na mila zao hapaswi kuridhi mali za mume waka paka atakapoolewa tena na kaka wa mume wake.

Vifo

Herbart anakufa kwa sababu ya kunywa pombe nyingi kwenye sherehe ya Cris inayomfanya adondoke na kupoteza maisha yake, Martha nae anakufa katika mgogoro wa kulinda mali za mumewe wake na pia katika kujitoa mikononi mwa George anayetaka kumuoa kwa lazima huku George akimlaani kwa kuendekeza sana mambo ya kisasa.

Hitimisho

Ni dhahiri kuwa maudhui ya kwenye ukingo wa thim ni makuu sana na ndomaana Ebrahim Hussein akakiita kitabu chake "kwenye ukingo wa thim". Maudhui mengine yanachangia pia kusababisha mvutano baina ya mila za zamani na usasa pia katika hali halisi ya wakazi wa wakazi wa Moshi maudhui ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa maishani mwao yamejaa chungu nzima yakiendelezwa na maudhui kama vile ndoa, migogoro, vifo, malezi kama ilivyo katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ameshughulikia muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti wake. Lengo kuu la mtafiti lilikuwa kuchunguza na kulinganisha hali ya mvutano ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ule katika jamii ya Wachaga mkoani Moshi.

5.1 Muhtasari

Uchunguzi ulifanyika katika vijiji vya Kibosho, Kibororoni, Mwika na Sambarai mkoani Moshi na iligunduliwa ya kuwa vijiji katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim ni sawa na vijiji vya utafiti wa mvutano baina ya Milan za zamani na usasa.

Data iliyokusanywa ilidhibitisha ya kuwa vyanzo vya mvutano wa mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim ni sawa na vyanzo vya mvutano baina ya umila na usasa katika vijiji vya utafiti.

Hali kadhalika taarifa ambayo mtafiti aliikusanya uwanjani ilibainisha kuwa watu wenye umri wa miaka kati ya kumi na tano hadi thelathini na mitano ndio wanaoshiriki kwa kiasi kikubwa katika muziki wa kisasa wa kichaga na usomaji wa vitabu vya fasihi mkiwemo Kiswahili.

Vilevile data iliyokusanywa inadhibitisha ya kwamba wengi wahojiwa wamewahi kukumbana na hali ya mvutano wa mila za zamani na usasa kwa namna moja au nyingine.

Pia data iliyokusanywa ilibainisha bayana kuwa suluhisho la mvutano baina ya mila za zamani limekuwa likitafutwa ilihali bado milango haijafunguliwa, hili limedhibitishwa na vipengele vya kijamii vinavyosawiri maisha katika jamii maalum. Vipenele hivi ni kama vile; majina, nyimbo, methali, misemo na vitendawili. Vipengele hivi husawili hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa mkoani Moshi.

Data ilidhiitisha bayana kuwa tamthilia ya kwenye ukingo wa thim ni kiwakilishi kamili cha hali ya mvutano baina ya umila na usasa mkoani Moshi, hii nikwasababu ya vyanzo na hali kamili ya umvutano baina ya mila za zamani na usasa ni vilevile. Kwahiyo jambo hili hutamatisha kuwa ilihali tamthilia ni kazi ya kubuni huwa ni kiwakilisho cha jamii halali. Ndio maana fasihi ni kioo cha jamii halisi.

Isitoshe data kutoka uwanjani ilidhihirisha kuwa mvutano baina ya mila na usasa ni jambo halisi na kwa ushahidi majina. Nyimbo na methali zao kwa kiasi kikubwa huzungumzia mvutano baina ya mila za zamani na usasa.

Fauka ya hayo data kutoka uwanjani huonyesha kuwa watu wengi katika jamii ya Wachaga wanapenda kusoma vitabu vya Kiswahili kwa sababu ndivyo vinavyopatikana kwa urahisi. Hii imejidhibitisha kwa hamu yao yakutaka kuchangia mengi kuhusu utafiti huu.

5.2 Hitimisho

Kulingana na matokeo ya uchunguzi huu, mtafiti alihitimisha kwa kusema kuwa mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim ni sawa na ule wa mkoani Moshi. Thibitisho la hitimisho hili ni mifano kadhaa ya visa vya mvutano wa mila na usasa mkoani Moshi, mifano hii nikama vile;

- Mvulana aliyeuliwa na ndugu wa msichana ambao walikuwa waarabu kwa kushindwa kuachana na dada yao wakati mila zao haziruhusu, hali hii ilitokea kijiji cha Sambarai
- Ndoa iliyokataliwa kufungwa na wazazi kijijini Mwika
- Mvutano uliotokea baina ya msichana na wazazi wake kijijini Kibosho

Pia katika majina, nyimbo, methali na misemo ya wachaga ambayo huwasilisha hali kamili ya jamii hiyo. Majina aliyokungua mtafiti ni kama yafuatayo;

- Namte- utengano
- Loishiye- sikuubaatika
- Namnyaki- hamna usawa
- Shigongo- ukombozi
- Kingunge- hawatutaki
- Alinainye- milele pamoja

Misemo iliyogunduliwa ni kama vile;

Eembe nenshisha- utandawazi ni jeanamu. Yaani utandadawazi wowote unaleta upotevu wa jamii lakini ufuataji wa mila na mbingu ya wanadamu

Nanshakulanyiwa emberoo- kilichokupa mwongozo ndo utakachokifuta. Msemo huu unaonyesha kama mila za zamani ndilizomfungua mtu macho ndoatakazofuata na kama usasa ndouliomfungua mtu macho ndoatakaoufuata.

Aidha kwa kipengele cha nyimbo pia mvutano baina ya mila za zamani na usasa husawiliwa.

Nyimbo hizi hubeba maana kwa ajili ya kuonya, kukuza utamaduni, kutangaza, kukashfu hali Fulani katika jamii. Kuna nyimbo zinazo sawiri hali ya mvutano wa mila za zamani na usasa mkoani Moshi kama vile;

- Nikusaidiaje- Profesor J
- Sizonje- Mrosho mpoto na Banana zoro
- Twende tukatambike mizimu- Wanne stars

5.3 Mapendekezo

Baada ya kuchunguza hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa katika tamthilia ya kwenye ukingo wa thim pamoja na hojaji, mahojiano na mapendekezo kutoka kwa wahojiwa, mtafiti alibaini mapendekezo kwa serikali, wanafunzi katika madaraja tofauti, jamii na familia zote. Mapendekezo ni kama yafuatayo;

Kwa serikali

Pendekezo kwa serikali ni kwamba kuundwe sheria zitakazolinda mipaka ya kimila na mipaka ya kisasa ili hali hizi mbili yaani hali ya kimila na hali ya kisasa zisiweze kuingiliana na kusababisha mvutano wowote ule katika jamii. Hili laweza kusaidia kupunguza kesi za mvutano wa kimila na kisasa mkoani Moshi

Kwa jamii

Kulingana na mwanamke mmoja "wazazi na wanajamii yapasa kuwaelewa watoto wao kwani huu niwakati wa utandawazi na ni senchari ya ishirini na moja"

Kuna mwanamke mmoja kutoka kijiji cha Mwika alipendekeza kamba " dunia imebadilika na hivyo jamii yapasa kutambua mabadiliko hayo na kwenda nayo ngazi kwa ngazi lakini pia jamii haipaswi kusahau kule ilipotoka yaani mila za desturi zake".

Mhojiwa mmoja alipendekeza kwamba wanajamii wapaswa kuheshimu mila na tamaduni walizozikuta kwani mila na desturi hizo ndio zitakazowaongoza katika maisha ya utandawazi ambayo yana mambo mengi sana.

Mapendekezo kwa familia

Mzee mmoja alipendekeza kuwa familia ifundishe watoto wao mila zao na tamaduni zao kuanzia wako utotoni hii itawafanya mamabo ya kisasa yasiweze kuwameza na familia inapaswa kuelewa kuwa maisha ya sasa sio kama yale ya zamani hivyo familia zinapaswa kuelewa mabadiliko ya kiutandawazi na kukubaliana na hali halisi.

Kwa upande wa mambo ya mahusiano mtaalam Prof Kitila Mkumba (2012) katika kitabu chake cha "Ndoa Tena" alisema kwamba " mila na tamaduni za kiafrika ni vizuri zikafwata lakini mila hizo hazistshili kuingilia hisia au mahusiano ya kimapenzi ya mtu kwani hisia ni kitu cha asili kilichoumbwa ndani ya mwili wa binadamu haviingiliani na mambo ya mila na tamaduni ingawa pale mtu anapofwata hisia zake watu husema anaiga mambo ya kisasa kitu ambacho sio kweli".

Prof Kitila aliendelea kuwa wapenzi wanapaswa kuvumilia kwa kujipa moyo na kujikaza kisabuni wakisimamia msimamo wa mapenzi yao. Familia pia inapaswa kutoingilia mahusiano ya watoto wao kwa kigezo cha kuendeleza mila na desturi zao kwani jambo hilo sio sahihi kabisa.

Jambo lingine la msingi ni kwamba ni bora kila familia ijue mipaka ya mila kwa watu wake wanaotakiwa kuifuata na pia familia inapaswa kuwapa elimu ya kutosha watoto wao juu ya mabadiliko ya kiutandawazi yanayoleta usasa katika maisha yao ya kila siku na namna ya kuenda sawa na mambo yote hayo mawili bila kuleta mvutano wowowte ule.

Mzee mwingine kijijini Mwika alisema kwamba ' vijana wanapaswa kuheshimu mawazo ya wazazi wao na hata wanafamilia pale wanapowaambia jambo lolote lile kwani busara ya wazee ni muhimu sana hasa katika kuendesha maisha ya usasa'

MAREJELEO

Gybser, N.C. AND Henderson, P.(2006). Comprehensive guidance and counseling programme basing on traditional and modernization aspects.http//www.tradcounselling. org,/files (04 April 2010)

1. Ludovick Joseph Rwezaura (2013) "Kilio Cha Mila Na Utandawazi".Imechapishwa na D.K Lunaningi

2. Norges Kristne Rad (PDF) (2009), "Mwili-Mmoja".

3. Rusell. B. Clayton Alexander, Nagurney (2014), "Love Chart", the love network,Cambridge University Press.

4. Dr. Ramadhani Rusavasula (2013), Betrayal with a purpose.Available at: http://www.nationalforum.com/electric%10jornal%30volumes/luneburg%20Fred (accessed 26 May 2013)

5. Andrew Noyes (2001), The Bitish scholars forum: Revising the factor endowment persepective on Afican traditional belief,1500-2000,, Traditional review history,61(3)

6. Gottam John (1986) University of Orgon:Modernisation in the continent, New York, Simon&Schuster.

7. Tanzania. Administrative Unit (Source: Tanzania Bureau Of Statistic) Geottive. Retrived 18 June 2013

8. Soanes, C.& Stevenson,A.(Eds).(2006)Concise Oxford Dictionary (11th ed). New York Oxford University Press

9. Masikini Prof. Kitila Mkumba (2012), Ndio basi tena.

10. JF-Expert Store. Complaints, Advance, Traditional and modernation Premier Members.

11. Jessica. R. Smith (2002). General Psychology: Behavior and social networking,http/www.webspace.ship.ed/cybour/limbicssystem/html (26 july 2009)

VIAMBATANISHO

A. Mwongozo wa hojaji

Jina langu ni Nannono Pauline mwanafunzi anayesomea shahada ya sanaa na elimu katika chuo kikuu cha Kampala International University. Ninafanya utafiti kuhusu uchunguzi linganishi wa mvutano kati ya ukale wa kitamaduni uliopo katika yamthilia ya kwenye ukingo wa thim na ule wa jamii ya wachaga mkoani Moshi. Kwahivyo naomba ujibu maswali haya kwa moyo mkunjufu na majibu yako yatahifadhiwa kama siri kabisa.

Asante sana.

1.a) Jina la kijiji.....

b) Jinsia.....

c) Una umri wa miaka mingapi (i) Miaka 15-24 ☐ (ii) Miaka 25-34 ☐

(iii) Miaka 35-44☐ (iv) Miaka mingine ☐

2. a) Umewahi kusikia au kushughulika na hali ya mvutano baina ya mila za zamani na usasa?

(i) Ndio ☐ (ii) Hapana ☐ (iii) Kiasi kidogo☐

b) Ikiwa jibu lako katika swali la (2a) hapo juu ni ndio, ni mvutano gani?

(i) Wa kimapenzi☐ (ii) Wakibiashara☐ (iii) Kirafiki☐ (iv) Kimilia

3. a) Umeshawahi kusikia nyimbo, methali na misemo inayozungumza juu ya mvutano wa kimila na kisasa?

i) Ndio☐ (ii)Hapana☐ (iii) Kiasi kidogo☐

b) Ikiwa jibu lako katika swali la (3a) hapo juu ni ndio ni nyimbo, methali au misemo ipi?

.....

.....

.....

4, Ni nini chanzo cha mvutano kati ya umila na usasa wa kitamaduni katika kijiji chako?

.....

.....

.....

5(a) Kuna uwezekano wowote wa kutatua shida hii?

i) Ndio ☐ (ii) Hapana ☐ (iii) Kiasi kidogo ☐

5(b) Ikiwa jibu lako hapo juu (5a) ni ndio, basi ni mbinu zipi zinazoweza kutumiwa kutatua shida hii?

.....

.....

.....

Asante sana.

B. Mwongozo wa mahojiano

Mimi ni Nannono Pauline mwanafunzi wa chuo kikuu cha Kampala International University. Ninafanya utafiti kutimiza baadhi ya mahitaji ya kuhitimu shahada ya sanaa ya elimu, kwa hivyo nawaomba ushirikiano wenu katika shughuli hii. Maoni yenu yataifadhiwa kwa siri kabisa.

(a) Jina la mjibu.....

(b) Jina la kijiji.....

(c) Umri wa wajibu.....

(i) 15-24 ☐ (ii) 25-34 ☐ (iii) 35-zaidi ☐

(d) Jinsia ya wajibu

(i) kiume ☐ (ii) kike ☐

2. Je umeshawahi kusikia au kushughulika na hali ya mvutano wowote wa kimila na kisasa?

(I) Ndio ☐ (ii) Hapana ☐ (lll) Kiasi kidogo ☐

3. Nini chanzo cha mvutano kati ya mila za ukale na usasa katika kijiji chako?

.....

.....

.....

4(a) Kuna uwezekano wowote wa kutatua shida hii?

(i) Ndio ☐ (II) Hapana ☐ (III) Kiasi kidogo ☐

4(b) Ikiwa jibu lako hapo juu 4(a) ni ndio, basi mbinu zipi zinazoweza kutatua shida hii?

.....

.....

Asante sana

C: PICHA ZILIZONASWA WAKATI WA KUKUSANYA DATA UWANJANI

Mwanakijiji wa kiboshokatika shughulizakila siku

WANAKE AKIELEZEAJINSI ALIVYOTENGWA NA FAMILIA YAKE

Babu akielezea jinsivijana walivyoaribikiwa na usasa